**22R-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy Al-Muthaqqal**

i. **الْمَدُّ اللاَّزِمِ الْحَرْفِيّ الْمُثَقَّل Al-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy Al-Muthaqqal**

Huitwa **الْمُثَقَّل** (al-muthaqqal - nzito) itakapokuja baada ya herufi ya madd, herufi inayoingizwa (idghaam) kwenye kinachokuja baada yake kusababisha shaddah; mfano katika kuitamka ل (laam) kwenye:

الٓمٓ ﴿١﴾ [1]

Inatamkwa: **اَلِفْ لآمْ مِّيمْ – alif laaaaaam-miym.**

**Bonyeza usikilize**

Herufi ya ل inaishia kutamkwa kwa مْ (miym saakinah) yaani: **لآمْ**(laaaaam). Kisha مْ hiyo ya saakinah imekutana na herufi ya م iliyo na i'raab na hivyo hapo hutokea idghaam na kusababisha shaddah. Ndio maana ikaitwa **الْمُثَقَّل** (al-muthaqqal - nzito); mfano pia:

طسٓمٓ ﴿١﴾ [2]

Inatamkwa **طا سِينْ مِّيمْ twaa siyyyyyyyn-mmiym**

**Bonyeza usikilize**

Herufi ya س (siyn) inapotamkwa, inaishia kutamkwa na نْ (nuwn saakinah). Kisha نْ hiyo imekutana na herufi ya م (miym) inayofuatia na kuifanya idghaam, na kusababisha shaddah. Ndio ikaitwa **الْمُثَقَّل** (al-muthaqqal- nzito).

---

[1] Al-Baqarah (2: 1)

[2] Ash-Shu'araa (26: 1)